East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-7 | Issue-12 | Dec- 2024 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2024.v07i12.003

OPEN ACCESS

**Original Research Article**

# Athari za Urazinishaji wa Wahusika Watoto katika Filamu za Kiswahili

Tuzo Peter Bitesigirwe[1*], Prof. Aldin K. Mutembei[2], Edith Lyimo[3]
[1]Mhadhri Msaidizi, Chuo Kikuu cha Dodoma
[2]Profesa Mshiriki, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
[3]Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Article History**
**Received:** 12.11.2024
**Accepted:** 17.12.2024
**Published**: 28.12.2024

**Journal homepage:**
https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Makala hii inahusu athari za urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili. Tafiti za kifasihi na kisaikolojia zinazohusiana na masuala ya watoto katika nyuga mbalimbali zinaonesha kuwa watoto wana urazini wa hali ya juu ikilinganishwa na umri wao. Katika uga wa fasihi, baadhi ya wataalamu wanabainisha kuwa urazinishaji wa wahusika watoto katika kazi za fasihi kama vile tamthiliya na vichekesho unabainika kutokana na matendo na lugha wanayotumia kuwa juu ya urazini wao. Filamu ni miongoni mwa kazi za fasihi zinazotumia wahusika watoto na hupendwa na hadhira pana ya watoto. Kwa hiyo, ni rahisi kwa wahusika watoto kujifunza mambo ambayo wakati fulani huwa nje ya uelewa wao na umri wao. Licha ya watoto kujifunza mambo yaliyo nje ya uwezo wao, bado uchunguzi kuhusu urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili haujapewa kipaumbele. Hali hii ikiachwa bila kuchunguzwa inasababisha kukosekana kwa maarifa kuhusu athari za urazinishaji kwa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili. Filamu zilizorejelewa ni za Steven Kanumba zilizotumia wahusika watoto. Filamu hizo ni *Ripple of Tears*, (2010), *This Is It* (2010), *Uncle JJ* (2010) na *Big Daddy* (2010). Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili kutoka kwa wahusika waliokuwa watoto katika filamu hizo (kwa sasa ni vijana), wazazi wa wahusika hao na mtunzi wa filamu hizo. Nadharia ya Saiko-Changanuzi iliyoasisiwa na mwanasaikolojia wa Kiswisi, Sigmund Freud (1856-1939) ndiyo iliyoongoza ukusanyaji na uchambuzi wa data za makala hii kupitia msingi wa ung'amuzi bwete. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna athari chanya na hasi za urazinishaji wa wahusika watoto kupitia filamu za Kiswahili. Athari chanya ni kukuza uwezo wa kufikiri kwa mhusika mtoto, chanzo cha kipato kwa mtoto na familia yake, hadhira ya watoto kuiga fanani ambaye ni mhusika mtoto. Aidha, athari hasi ni pamoja na athari za kisaikolojia, mhusika mtoto kujengewa mtazamo hasi kwenye jamii, changamoto za ukuaji kutoka utotoni hadi utu uzima na kuandikwa vibaya na vyombo vya habari. Makala hii pia imetoa mapendekezo.

**Keywords:** Urazinishaji, Filamu, Watoto.

**Copyright © 2024 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Dhana ya urazinishaji inaweza kufafanuliwa kulingana na muktadha uliotumika kuiibua. Miongoni mwa miktadha ambayo dhana hii hutumika ni saikolojia na fasihi. Baadhi ya wataalamu katika uga wa fasihi wanafafanua kuwa urazinishaji ni istilahi inayotumiwa kurejelea mchakato wa kumtanabahisha na kumzindua mtu kiakili ili aweze kujijua na kujitambua (Okereke, 1997; Mumbo, 2013 na Ekiru, 2018). Uzinduaji huo unaenda sambamba na kupandikiza maarifa mapya katika akili ya mtu. Kwa hiyo, katika makala hii dhana ya urazinishaji inarejelea mchakato wa kumpandikizia mtu maarifa mapya. Urazinishaji katika fasihi unaweza kuangaliwa katika tanzu zote za fasihi ikiwamo filamu. Filamu ni fasihi iliyoibuka kutokana na maendeleo ya teknolojia katika uwasilishaji na uhifadhi wake (Mlaga, 2017; Kasiga, 2022). Kutokana na kupendwa na hadhira pana (Kasiga, 2022) filamu nyingi hutumia wahusika mchanganyiko, yaani watu wazima na watoto, katika kuwasilisha maudhui yake kwa jamii. Katika filamu nyingi, watoto hupewa uhusika unaobatilisha wema walionao (Traverso, 2005). Maelezo haya yanamaanisha kuwa mtoto anaweza kuwa hajui kuhusu wizi lakini filamu humtaka avae uhusika wa wizi. Kwa hiyo, mhusika huyu atakuwa amepata maarifa juu ya wizi.

Kutokana na maelezo haya urazinishaji wa watoto unaenda sambamba na kuwapandikiza watoto maarifa ambayo hawakuwa nayo awali. Wahusika watoto katika filamu wanaweza kujengewa uhusika wao kupitia lugha wanayotumia, mavazi na matendo yao katika kufikisha ujumbe. Vipengele hivi huwarazinisha wahusika watoto kwa kuwa baadhi ya maudhui huwa juu ya urazini wa umri wao.

Wataalamu wa filamu na saikolojia wanadai kuwa wahusika katika filamu wanapata athari mbalimbali za kisaikolojia na kijamii kutokana na maudhui wanayoyawasilisha (Currie na Wasylkiw, 2011; Seng na Wenzake, 2013). Wahusika watoto ni miongoni mwa waigizaji katika filamu za Kiswahili. Watoto hawa hupewa uhusika unaotokana na mahitaji ya mtunzi. Kwa kawaida, urazini wa watoto ni mdogo ukilinganishwa na wa watu wazima (Ngugi na Wenzake, 2019) hivyo, ni rahisi kurubuniwa na vipengele vya kuvutia vya kiutandawazi. Hali hiyo huwasababisha kuyumbishwa kutokana na mabadiliko wanayokutana nayo. Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa watoto wanaweza kupoteza mwelekeo sahihi na kuathiri urazini katika maisha yao. Pamoja na tafiti hizo kuwa muhimu katika jamii, suala la urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu halipewi kipaumbele. Makala hii imechambua na kuwasilisha athari za urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu tano za Kitanzania zilizohusisha wahusika watoto. Makala hii imegawanywa katika sehemu tano; sehemu ya kwanza inahusu utangulizi ambao unaeleza azma ya makala hii. Sehemu ya pili inaelezea nadharia iliyoongoza uchambuzi wa data, sehemu ya tatu ni methodolojia za utafiti. Sehemu ya nne ni uchambuzi wa data na mjadala na sehemu ya tano ni mapendekezo na hitimisho.

## 2.0 METHODOLOJIA YA UTAFITI

Data za makala hii zilikusanywa kwa njia ya mahojiano kwa kurejelea filamu nne (4) za Steven Kanumba zenye wahusika watoto ambazo ni *Ripple of Tears* (2010), *This Is It* (2010), *Uncle JJ* (2010) na *Big Daddy* (2010). Filamu hizo zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Aidha, filamu za Steven Kanumba ziliteuliwa kutokana na kuwavisha watoto uhusika ulioibua maudhui halisi ya Kitanzania. Upatikanaji wa data hizo ulifanyika uwandani kwa kutumia njia ya mahojiano. Mahojiano yalifanyika kwa makundi matatu ambayo ni wahusika watoto katika filamu teule (kwa sasa ni vijana), wazazi watatu wa wahusika watoto na watayarishaji wa filamu hizo. Watoa taarifa hao wamepewa msimbo kulingana na hadhi zao. Mathalani, kundi la wahusika watoto limepewa msimbo wa mhusika mtoto kuanzia namba 1 hadi 3 (MT), kundi la wazazi limepewa msimbo wa mzazi wa mhusika mtoto kuanzia namba 1 hadi 3 (MMT) na kundi la watayarishaji wamepewa msimbo wa mtayarishaji wa filamu (MF). Data zilizokusanywa kutoka kwa watoa taarifa ziliwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli.

### 3.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Saiko-Changanuzi. Nadharia hii iliasisiwa na mwanasaikolojia wa Kiswisi, Sigmund Freud (1856-1939) aliyekuwa tabibu wa magonjwa ya akili. Bidii yake katika kutibu wagonjwa ilimfanya aanze kutafiti sababu za matatizo ya akili kwa wagonjwa wake. Freud aligundua kuwa katika akili ya binadamu kuna sehemu ya unga'muzibwete ambayo huratibu fikra, mawazo, hofu, mitazamo, wasiwasi, matamanio na matarajio ya mtu ambayo hayawezi kujitokeza waziwazi bali kwa njia ya ndoto (Freud, 1915). Aidha, Freud aligundua kuwa mwenendo wa mwanadamu huathiriwa na matukio mbalimbali aliyoyapitia katika kipindi cha utotoni. Mawazo ya mtaalamu huyu yalitumiwa na wataalamu mbalimbali katika taaluma za sosholojia, filosofia, fasihi na nyinginezo. Katika fasihi, Holland (2012) anadai kuwa wahusika wanaopatikana katika kazi ya fasihi wanatokana na mawazo ya king'amuzibwete kama vile ndoto na matamanio ya mtunzi. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kuwa katika utunzi wa filamu, mtunzi anaandaa filamu na kujenga uhusika kwa kuzingatia mahitaji na matamanio yake. Kwa mantiki hiyo, wahusika watoto katika filamu wanarazinishwa kulingana na mahitaji ya mtunzi. Mawazo ya nadharia hii yalitumika katika kubaini athari za urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu teule.

## 4.0 UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Sehemu hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizopatikana katika filamu teule za Steven Kanumba. Uwasilishaji na uchambuzi wa data uliongozwa na mhimili wa Nadharia ya Saiko-Changanuzi kama ulivyodokezwa hapo awali. Utafiti uliozaa makala hii umebaini kuwa kuna athari chanya na hasi za urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili. Athari chanya zilizobainika ni kukuza uwezo wa kufikiri kwa mtoto, kupata fedha, hadhira ya watoto kuiga fanani ambaye ni mtoto. Pia, athari hasi zilizobainika ni athari za kisaikolojia, changamoto za ukuaji, mhusika mtoto kupewa mtazamo hasi katika jamii na kuandikwa vibaya katika vyombo vya habari. Athari hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo;

### 4.1 Athari Chanya za Urazinishaji wa Wahusika Watoto katika Filamu za Kiswahili

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili una athari chanya kwa wahusika watoto. Athari zilizochambuliwa na kuwasilishwa katika sehemu hii ni zile za baada ya filamu kuigizwa. Aidha, data zilikusanywa kutoka kwa waliokuwa wahusika watoto katika filamu teule, wazazi wa waliokuwa wahusika watoto pamoja na watayarishaji wa filamu husika. Athari hizo zimechambuliwa na kuwasilishwa kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Kukuza Uwezo wa Kufikiri kwa Mtoto

Utafiti wa makala hii umebaini kuwa miongoni mwa athari chanya ya urazinishaji wa wahusika watoto

katika filamu teule ni kukuza uwezo wa kufikiri. Kukua kwa uwezo wa kufikiri kwa wahusika watoto kumebainishwa katika filamu teule kutokana na ukweli kwamba wahusika watoto katika filamu teule wameanza kazi ya kuigiza katika umri wa miaka mitano hadi kumi (5-10). Piaget (1970) anaeleza kwamba umri huu ni muhimu kwa kukuza uwezo wa kufikiri wa mtoto. Hivyo, linapokuja suala la mtoto kuigiza katika filamu kuna namna mbalimbali ambazo uhusika wake unaacha athari chanya katika maendeleo ya uwezo wake wa kufikiri. Mtoto huweza kukuza uwezo wake wa kufikiri kupitia kukumbuka mistari ya maneno magumu anayokuwa amepewa, kuelewa hisia anazotakiwa kuziwasilisha, kupangilia jinsi ya kuongea kwa hisia na vitendo. Suala hili lilithibitishwa na mtoataarifa MT 2 aliposema;

Nilitumia muda mwingi kukariri yale maneno niliyopewa kwenye *Uncle JJ* pamoja na *This Is It*. Wakati wa kuigiza *Uncle JJ* sikusumbuka sana kwani nilikuwa nimeshajua namna ya kukariri na kucheza na hisia za mwili wangu(Chanzo, mahojiano na MT 2, 25/1/2024).

Dondoo hili linaonesha jinsi mhusika mtoto alivyokuwa anatumia muda mwingi katika kufanikisha kile anachopewa kuwasilisha. Hali ya kukariri maneno kama ilivyoelezwa na mtoataarifa humwongezea mtoto uwezo wa kufikiri kiasi cha kuuvaa uhusika anaopewa katika kazi husika ya kifasihi (Hunt, 1999). Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa suala la uigizaji linahusisha kuvaa uhusika zaidi ya jinsi mtu alivyo, kwa hiyo, inahitaji kufikiri sana ili kuweza kuendana na uhusika anaouvaa. Vilevile, athari hii imethibitishwa na mtoa taarifa MT 1 anayesema:

Uhusika ni nafsi yako nyingine ambayo huijui na unaiingia pale unapopewa kuigiza nafasi husika. Kwa hiyo, inahitaji sana ujue namna ya kufikiri kujitoa nafsi yako na kuvaa nafsi ya uhusika unayopewa. Hata kama unaona umekosea wakati wa kuigiza inatakiwa ufikiri harakaharaka jinsi ya kufunika hilo kosa. Uwezo nilioupata huko (nikiwa mdogo) ulinisaidia sana hadi sasa ninakubalika katika tasnia ya filamu na ninapata kazi (Chanzo; mahojiano na MT 1, 27/11/2023).

Dondoo hili linaonesha jinsi mhusika mtoto anavyotumia akili yake kufikiri namna ya kuvaa uhusika anaopewa. Kuvaa uhusika kunahitaji sana uwezo wa kufikiri wa namna gani uvae uhusika tofauti na uhalisia ulionao. Hali ya mhusika mtoto kuuvaa uhusika usio wake humwezesha kukuza uwezo wa kufikiri na namna ya kukabiliana na mazingira yanayomzunguka (Ngugi, 2016). Kutokana na hoja hii, wahusika watoto wana nafasi kubwa ya kukuza uwezo wao wa kufikiri na kukumbuka hususani wanapokuwa wanajitahidi kukariri yale wanayotakiwa kuwasilisha. Aidha, mazoezi ya kukariri na kukumbuka wanayoyafanya mara kwa mara huwafanya wajiamini na kuendelea kupata kazi mbalimbali za kuigiza. Mwanasaikolojia Beebe (2004) anadai kuwa mazoea ya mara kwa mara hujenga tabia. Mawazo haya yanathibitisha kuwa mambo mbalimbali anayoyapitia mtu yana athari katika maisha yake.

#### 4.1.2 Chanzo cha Kipato kwa Mhusika Mtoto na Familia Yake

Miongoni mwa dhima za filamu kama fasihi iliyostawi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ni kuburudisha, kuelimisha na kuasa (Mlaga, 2017; Kasiga, 2021). Pia, filamu inasaidia katika kukua na kuongeza kipato cha taifa na mtu mmoja mmoja hususani watunzi wasambazaji, waongozaji na waigizaji kwa ujumla. (Mwakalinga, 2013). Utafiti huu umebaini kuwa kupitia urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu teule, watoto hujipatia fedha na hivyo kuongeza kipato katika familia zao. Mara nyingi kipato hicho huwasaidia watoto kulipia ada zao za shule na kuwasaidia wadogo zao. Haya yanathibitishwa na mtoataarifa MM1 anaposema;

Baada ya kuelewa nilichokuwa natakiwa kufanya katika filamu kutokana na niliopewa, bosi alinipenda na hivyo kuanza kunilipa vizuri zaidi. Pesa zangu nilikuwa nampatia mama baadae alinitafutia shule nzuri ambayo nilisoma hadi kumaliza darasa la saba. Nilipofaulu kwenda sekondari tayari nilikuwa na hele ya kutosha kulipia shule nzuri ya binafsi hivyo sikuhangaika sana (Chanzo; mahojiano na mtoataarifa MT1, 27/11/2023).

Dondoo hili linaonesha kuwa wahusika watoto hujipatia kipato kinachoawezesha kukidhi mahitaji yao pamoja na gharama za shule. Si tu hilo bali kipato hicho huwa muhimu katika kuendeleza uchumi wa familia zao. Mtoataarifa anathibisha;

Kwa kuwa nilikuwa mtoto, nilikuwa sijui ninapata kiasi gani cha pesa lakini mama alikuwa ananitunzia pesa zangu na wakati mwingine anatumia katika mahitaji ya kifamilia akikwama, lakini kadiri nilivyokuwa nakua nilikua naona pesa ninayoipata. Baadae nilifunguliwa akaunti benki, na hadi sasa hivi naendelea kupata hela nakutunza hela yangu mwenyewe (Mahojiano na mtoa taarifa MT 2, 25/1/2024).

Dondoo hili linaonesha kuwa wahusika watoto wanasaidia kuinua hali ya kiuchumi katika familia zao. Kutokana na hali hii watoto hujikuta wanatia bidii katika kazi wanayopewa ili kuendelea kupata kiasi cha pesa zaidi.

Suala hili linajadiliwa pia na Risinger (2017) kuwa waigizaji watoto mara nyingi wanakuwa katika hatari ya kufanya kazi kwa bidii na katika mazingira hatarishi kwa mtoto. Mtaalamu huyu anataja mazingira hayo kuwa ni pamoja na matamasha ya usikuna safari za ghafla zinazoingilia ratiba ya masomo ya mtoto. Hata hivyo, utafiti huu umebaini kuwa nchini Tanzania watoto wengi waigizaji bado wako chini ya usismamizi wa wazazi wao kwa hiyo husimamiwa na wazazi kwa

kushirikiana na waajiri wao ili kumfanya mtoto afurahie maisha yake ya uigizaji.

Sambamba na hilo, utafiti huu umebaini kuwa kusimamia mapato kunaweza kuwa changamoto kwa mtoto hivyo wanahitaji uangalizi makini ili kuzuia ufujaji na unyonyaji kutoka kwa wasimamizi wao. Watoto wengi wanaodhulumiwa hupata matatizo ya msongo wa mawazo, kupoteza imani kwa mtu yeyote na kukata tamaaa ya kuendeleza kipaji chake. Data ifuatayo inathibitisha;

Ninakumbuka mkataba wa kwanza kabisa wa mimi kuanza uigizaji ulisaniwa na rafiki yake mama na ndiye alikuwa akinisimamia. Ila kuna kipindi nilikosa ada ya shule ikabidi mama akafuatilie kwenye kampuni husika. Yaani huwezi amini, alioneshwa listi zote za malipo yangu kuanzia mwezi nilioanza. Baadae mama aligundua kuwa nilikuwa nadhulumiwa na huyo rafiki yake, basi tukavunja mkataba na kuanza upya mwingine. Nilivyoambiwa hali hiyo nilijisikia vibaya, sikutamani hata kuendelea kuigiza tena lakini baadae mambo yalienda vizuri.(Chanzo, mahojiano na MT 1, 27/11/2023).

Maelezo haya yanaonesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa wahusika watoto kufanyiwa dhuluma, hali inayoweza kuwakatikasha tamaa ya kuendelea kujihusisha na filamu. Kutokana na hali hii Nchini Marekani katika jimbo la Califonia ilitungwa sheria ya kuwasimamia waigizaji watoto iitwayo *Coogan Law* [1]. (Gaydos, 2023) ambayo inawasaidia watoto kutunza asilimia 15 ya mapato yao ili wanapofikia umri wa utu uzima mapato hayo yawasaidie katika kukabiliana na changamoto za kimaisha na kuepusha msongo wa mawazo kwa watoto.

Tafiti zinaonesha kuwa kuanzia mwaka 2005 hadi sasa watoto wamekuwa akiingizwa katika tasnia ya sanaa kama vile filamu, vichekesho na muziki. Kutokana na urazini wa watoto kuwa mdogo katika masuala ya maslahi na haki zao, watoto wengi wanasimamiwa na wazazi au ndugu wa karibu. Utafiti huu unapendekeza kuwa ni wakati mwafaka sasa wa serikali na taasisi za sanaa kutunga sheria kwa ajili ya kusimamia maslahi ya watoto kwa ajili ya ustawi mzuri wa sanaa yenye tija hapo baadae. Aidha, utafiti huu unapendekeza kuwa zimekuwepo sheria mbalimbali za kudhibiti na/au kulinda maadili, saikolojia na makuzi ya watoto kwa mfano, sheria za kudhibiti ukatili kwa watoto, mahusiano ya kimapenzi, matumizi ya pombe na sigara. Sheria kama hizi zinaweza kuimarishwa katika kulinda hadhi ya wahusika watoto katika sanaa.

**4.1.3 Hadhira ya Watoto Kuiga Fanani ambaye ni Mhusika Mtoto**

Watoto wengi hupenda kujifunza kupitia watoto wenzao. Kwa hiyo, wahusika watoto wanapokuwa wanawasilisha maudhui yao, hadhira hasa ambao ni wenzao (watoto) si rahisi kutofautisha uhalisia na uigizaji. Mathalani, mhusika mtoto katika filamu ya *Uncle JJ* alipata wafuasi wengi na kila alipopita watoto wengi walimfurahia na kumfuata. MT 2 anasema:

Sikujua kama itakuwa hivi. Baada ya filamu ya *Uncle JJ* kutoka, niliona
watoto wengi wananifuata. Nikiwa shule wanafunzi hadi wa jirani walikuwa
wakija kunitazama na kujifunza jinsi nilivyokuwa naongea kwenye filamu (Chanzo, mahojiano na MT 2, 25/1/2024).

Dondoo hili linaonesha kuwa hadhira ya watoto huiga mambo mengi kutoka kwa wahusika watoto. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa urazinishaji wa mhusika mtoto unasababisha hadhira ya watoto kuiga tabia za wahusika watoto. Mathalani, hadhira anaweza kupenda msimamo wa mtoto, hali ya kutetea haki zake na uwajibikaji wake katika masomo. Aidha, kutokana na tabia mbaya ambayo mhusika mtoto anapewa kuigiza katika filamu mathalani, tabia ya ukorofi, jeuri na matumizi ya maneno machafu, moja kwa moja huathiri hadhira inayomfuatilia kiasi cha kumjengea taswira mbaya mhusika mtoto. Kwa mantiki hiyo, watunzi na waandaaji wanapaswa kuzingatia mambo muhimu ya kuyapa makini wakati wa uandaaji wa uhusika wa watoto. Akizungumzia mambo yanayopewa makini katika kuandaa uhusika wa watoto, mtoataarifa ambaye ni MF 1.

Unapoandaa uhusika wa mtoto ni lazima uzingatie pia watoto wengine watakaomtazama. Mfano, ukitunga habari inayohusu mtoto mkorofi ni muhimu kuonesha chanzo cha huo ukorofi na mwisho wa huo ukorofi ili watoto wengine wasijekudhani ukorofi ni sifa nzuri. Kwa hiyo, kunapaswa kuwepo na mwisho unaoonesha tabia njema. (Chanzo: mahojiano na MF 1, 10/1/2024).

Nukuu hii inadhihirisha kuwa baadhi ya tabia wanazoigiza wahusika watoto huwapelekea kuwa na mwisho mbaya katika familia na jamii. Kwa hiyo, urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu unapaswa kuzingatia maadili na sheria zinazolinda haki za watoto. Pia, haki hizo zizingatie pia watoto watazamaji ili wasiweze kuathirika kisaikolojia. Wanasaikolojia wengi wanaamini kuwa kutazama tabia fulani isiyofaa mara kwa mara kama ukatili, ngono na ulaghai kunaweza kuleta mmomonyoko wa maadili miongoni mwa watoto. Hivyo, ni muhimu kwa watunzi kuwarazinisha wahusika watoto maudhui yanayofaa kwa jamii na ikitokea ni

[1]Sheria hii ilipitishwa jimboni Califonia mwaka 1939 ili kulinda haki za mapato za waigizaji watoto. Hali hii ilitokea baada ya muigizaji mtoto Jackie Coogan aliyejipatia mamilioni ya dola za Kimarekani lakini baadae ilibainika kuwa hadi kufikia utu uzima wake (miaka 18) hakuwa na hela yoyote kwa sababu mama na baba yake wa kambo waliivuja (Gaydos, 2023).

muhimu kwao kuwasilisha yale yaliyokusudiwa kuibadilisha jamii waoneshe mwisho ulio mwema.

Sera ya nchi ya Tanzania ambamo tasinia ya filamu maarufu kama *Bongo Movie* inayoonekana kuimarika bado inathamini maadili ya Mtanzania na kusisitiza wahusika wake waigize maudhui yanayosadifu hali ya Mtanzania ili kuwaokoa watoto ambao wengi ni hadhira yao. Akizungumzia umuhimu wa kuwarithisha watoto mambo mazuri kwa ajili ya kizazi kijacho, Mlama (2003) anasema kuwa kufikia utu uzima, watoto wasitazamiwe kufurahia na kuthamini utamaduni wao ikiwa hawakuwahi kushughulishwa na umuhimu wa uadilifu. Kwa mujibu wa nadharia ya Saiko-Changanuzi, Freud (1915) anadai kuwa uzoefu wa maisha ya mtu utotoni ndio unaomfanya kuwa jinsi alivyo ukubwani. Maelezo haya yanaonesha kuwa ni muhimu watoto kufundishwa na kuzoezwa kuona mambo mazuri katika kipindi cha utoto wao ili wakiwa wakubwa waweze kuyaishi. Kadhalika, hadhira ya watoto inapaswa kufurahia, kuelimika na kujifunza kupitia wahusika wazuri wanaowaona. Kwa mantiki hiyo, makala hii inasisitiza kuwa ni muhimu kujenga kizazi kijacho kwa kuanza na kilichopo. Hivyo, ni vyema kuwarithisha watoto mambo mema ili kutengeneza jamii njema ya kesho.

### 4.2 Athari Hasi za Urazinishaji wa Mhusika Mtoto katika Filamu Teule za Kiswahili

Sehemu hii imechambua na kuwasilisha athari hasi za urazinishaji kwa wahusika watoto katika filamu teule za Kiswahili. Athari hizi ni zile ambazo husababisha mtu kuingia kwenye mgogoro binafsi wa kisaikolojia, kijamii au kiutamaduni (Sanga, 2020). Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa urazinishaji wa mhusika mtoto katika filamu teule una athari hasi tofauti na athari chanya zilizojadiliwa hapo juu. Aidha, uchambuzi na uwasilishaiji wa data katika sehemu hii umeegemezwa katika data zilizokusanywa uwandani. Athari zilizojadiliwa ni kama zifuatazo:

#### 4.2.1 Athari za Kisaikolojia

Utafiti huu umebaini kuwa miongoni mwa athari hasi za urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu teule ni athari za kisaikolojia. Athari za kisaikolojia zinarejelea athari zinazogusa fikra za mtu hata kumbadilisha kimtazamo, kimawazo na kivitendo. Kwa kawaida, urazini wa watoto ni mdogo (Ngugi, Lyimo na Bakize, 2019) ukilinganishwa na wa watu wazima, hivyo, wanategemea kushibishwa na mambo yanayoendana na umri wao. Kushibishwa na mambo yaliyo juu ya urazini wao inaweza kuchukuliwa kama mtu aliyekula chakula kingi kuliko uwezo wa tumbo lake na baadaye kuvimbiwa au/na kupasuka (Currie na Wasylkiw, 2011). Vivyo hivyo, kwa watoto wanaonasa mambo yaliyo juu ya urazini wao wanaweza kuvimbiwa; na athari huonekana katika matendo na mwenendo wa maisha yao ya kila siku. Akijibu swali la mambo ya kuzingatia katika kuandaa wahusika watoto kwa ajili ya uigizaji, mtoa taarifa MF 2 anasema;

Ni kweli watoto kwa asili wanaiga. Watoto wanaweza kuiga mambo ambayo yanafanyika wakati wa uigizaji na wakadhani ndiyo maisha halisi ya waigizaji. Kwa hiyo, tunachozingatia ni kuwa makini. Kuna wakati mnaweza kuwa katika nyakati za kawaida ambazo hazihusiani na filamu lakini ukamwona mtoto anaongea kama yuko kwenye filamu (Chanzo, mahojiano na mtoa taarifa MF 2, 16/10/2023).

Maelezo haya yanaonesha jinsi mhusika mtoto anavyoweza kuathirika kwa kuona tabia au mambo yanayoendelea wakati wa uandaaji na uigizaji wa filamu. Hoja hii inamaanisha kwamba kisaikolojia ni rahisi mtoto kuathiriwa kutokana na maudhui mbalimbali anayoyawasilisha. Sambamba na hayo, wahusika watoto wanaoigiza mara kwa mara maudhui yaliyopevuka tofauti na umri wao kama vile uhalifu, mahusiano ya kimapenzi, wivu na migogoro mbalimbali, wanawahi kuingia katika hali ya utu uzima. Athari hizo za kisaikolojia humwelekeza mtoto kuweza kufanya vitu ambavyo vinaweza kuwa kinyume na utamaduni wa jamii husika. Sambamba na hayo mhusika mtoto akikosa usimamizi mzuri wakati na baada ya uigizaji basi anaweza kupata athari zinazoweza kubadili mwenendo na tabia yake.

Ama kuhusu mabadiliko ya tabia, Bicard (2012) anaeleza kuwa tabia ni hali ambayo inafanywa na mtu ambayo inaweza kuonekana, kupimwa na kurudiwa. Kwa mantiki hiyo, tabia za wahusika watoto zinapoharibika zinaweza kupimwa na kuonekana katika maisha yao halisi. Urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili unachangia kwa kiasi kikubwa kuharibika kwa tabia za wahusika watoto. Mtoataarifa MF anaeleza kuwa kuna mazingira kama vile ya ulevi yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha kuharibu saikolojia ya mtoto kiasi cha kuifanya tabia ya mtoto ibadilike. MF 2 anaendelea kueleza kuwa:

Inapotokea mtoto ameshiriki katika *scene* inayohitaji kwenda kwenye maeneo ya ulevi inabidi umakini uongezeke ili mzazi ajue anamkabidhi mtoto kwa nani ili baadaye asije kujilaumu. Vilevile, wanadamu hatufanani, hivyo, mzazi anapaswa kuwa mtu wa kwanza katika kuchukua tahadhari dhidi ya mtoto hata kama ya kumkabidhi kwa watu anaowaamini (Chanzo: Mahojiano na mtoataarifa MF 2, 10/1/2024).

Dondoo hili linaonesha kuwa urazinishaji wa mhusika mtoto katika filamu teule una athari hasi kwa sababu tabia ya mtoto inaweza kuharibika kutokana na uhusika wao (lugha, maleba, vitendo na muktadha). Hali hii husababisha athari kubwa kisaikolojia kwa mtoto kiasi kinachoweza kumbadilisha tabia yake kuwa kinyume na maadili ya jamii (Buckingham, 1997). Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa uhusika wao unaweza kuwa chanzo kikubwa cha mhusika mtoto kuwa na tabia ambazo hakuwa nazo hapo awali. Mathalani, mtoto anaposhiriki katika maeneo ya ulevi na washiriki wenzake au kuigiza kipengele cha ulevi ni rahisi kwa

mhusika huyo kujiingiza katika ulevi. Utafiti uliofanywa na Currie na Wasylkiw (2011) pamoja na Seng na wenzake (2013) ulibaini kuwa wahusika watoto katika filamu za Kikorea na Kimarekani wanapofikisha umri wa ujana na utu uzima wanakuwa wameathirika kisaikolojia kutokana na masuala ya vurugu na ukorofi wanayoyaigiza mara kwa mara. Athari zao huenda mbali na kuwa watumiaji wazuri wa madawa ya kulevya na uhalifu uliokithiri.

Kutokana na athari hizo za kisaikolojia kwa wahusika watoto ni jukumu la wazazi na walezi kuhakikisha kuwa mhusika mtoto haathiriwi kisaikolojia na maudhui anayoyawasilisha. Katika utafiti wa Seng na Wenzake (2013) inashauriwa kuwa ni vyema wahusika watoto wapewe ushauri nasaha kabla na baada ya kuigiza ili kuwaondolea kiwewe na athari nyingine za kisaikolojia watakazozipata wakati na baada ya uigizaji. Watafiti hawa wanasisitiza hilo kwa kutolea mfano kupitia shirika la filamu la Califonia ambapo *Hollywood* imeshika mizizi, kuwa ni vyema kuwepo kitengo maalumu cha kuangalia mazingira ya watoto waigizaji ili wapewe msaada wa kisaikolojia pale inapotakiwa. Nchini Tanzania watoto wengi wamekuwa wakitambulishwa katika uigizaji wa filamu za Kiswahili jambo ambalo ni jema kwa kuzingatia lengo zuri la tasnia ya filamu katika kukuza na kuzalisha vipaji vya watoto, lakini ni muhimu kwa watoto hawa kupewa msaada wa kisaikolojia panapohitajika. Mathalani, akifafanua tabia husika ambazo hakupenda mwanae apatiwe wakati wa uigizaji, MMT 2 anasema:

Kiukweli sikupenda mwanangu ahusishwe na uhusika wa ulevi, ujambazi na wizi. Mwanangu alivyo, nilipenda ahusike hivyo hivyo ili aendelee kukua katika misingi ya imani na dini niliyomlea. Unajua mimi ni muigizaji, na huko kuna mambo mengi, ukishamtambulisha mwanao katika uigizaji basi ujiandae kukaa naye mara kwa mara kumweleza kuhusu misingi anayotakiwa ili kukabiliana na changamoto zinazotokana na uigizaji (Chanzo; mahojiano na MMT, 27/11/2023).

Dondoo hili linadhihirisha jinsi suala la uhusika wa watoto ni tata hata kwa wazazi wao na jamii inayowazunguka. Utata huo unadhihirisha kuwa uhusika wanaopewa wahusika watoto huwa na athari hasi hususani katika makuzi yao. Kadhalika, utafiti huu umebaini kuwa mzazi ana jukumu la kwanza kuhakikisha anakabidhi mtoto wake watu ambao wataweza kumjenga katika maadili mema. Mtoataarifa MMT 3 anaeleza:

Hivi unajua sisi wazazi wa wasanii wa *Bongo movies* kuna wakati tunaogopa kujitokeza kutokana na matukio wanayowahusisha watoto wetu. Yaani, unakuta mzazi hajivunii mtoto wake kuwa maarufu. Wasanii wa bongo *movies* (aliwataja baadhi) wanajulikana kwa kudanga (kuingia kwenye mahusiano mbalimbali kwa lengo la kupata mali) kugombania wanaume, kupiga picha chafu, yaani utafikiri usanii hauwalipi. Sasa mazingira kama hayo utamruhusuje mwanao kuwa msanii? Ndiyo maana mimi kila siku namshauri mwanangu ajitahidi asiwe kama wakubwa zake walio katika tasinia hii na ninashukuru ananisikiliza (Chanzo, mahojiano na MMT 3, 25/1/2024).

Maelezo haya yanaonesha wasiwasi wa mzazi unavyojitokeza kupitia uigizaji wa wahusika katika filamu teule za Kiswahili. Aidha, mahojiano haya yanaonesha kuwa baadhi ya waigizaji wa filamu za Kiswahili wamekuwa na matukio mengi ya kushangaza na ya kuhuzunisha kiasi cha kuondoa ile dhana ya kuwa msanii ni kioo cha jamii. Suala hili linamaanisha kuwa jamii haijitazami, haijirekebishi wala haibadiliki kupitia msanii. Badala yake, kutokana na msanii baadhi ya wanajamii wametumbukia shimoni kwa kuiga matendo yasiyofaa kwa msanii huyo. Akizungumzia suala la kutokuwa kioo cha jamii kwa wasichana wadogo waliopaswa kumtazama na kujifunza kwake MT 3 anasema;

Maudhui niliyopewa niyawasilishe, niliyawasilisha vizuri na uhusika niliuvaa vizuri. Watu wengi walinipenda na nikawa maarufu. Si uigizaji wa filamu unaomfanya mtu kubadili tabia bali ni kuwa umaarufu unakuja na changamoto nyingi. Mara nyingi watu wanaopata umaarufu katika umri mdogo wanapokosa msaada wa kisaikolojia lazima wapotee kutokana na jinsi jamii inavyowapokea. (Chanzo: Mahojiano na MT 3, 5/3/2024).

Maelezo haya yanaonesha dhahiri kuwa kunahitajika msaada wa kisaikolojia kwa wahusika watoto kabla na baada ya kuigiza maudhui fulani ambayo yanawapatia umaarufu ambapo kutokana na umaarufu huo wanashindwa kuhimili misukosuko wanayoipata katika jamii na hivyo kuonekana si vioo vya jamii.

Kutokana na maelezo haya, ni muhimu kwa mzazi kuwa makini katika kumruhusu mtoto anapokwenda kuigiza, kwani kuna mambo mengi anaweza kukumbana nayo. Sambamba na hayo, ni muhimu kwa waliokabidhiwa watoto hao kuwa makini na waaminifu ili kutimiza lengo na ndoto za watoto.

### 4.2.2 Changamoto za Ukuaji Kutoka Utotoni Hadi Utu Uzima

Suala la ukuaji wa watoto limejadiliwa na wataalamu mbalimbali wa saikolojia za ukuaji. Wataalamu hawa wamegawa vipindi vya ukuaji wa mtoto katika makundi mbalimbali ya umri na mahitaji ya mtoto kiumri. Mathalani, Piaget anaeleza kuwa kundi la kwanza ni la watoto kuanzia umri wa miaka 0 hadi 2. Watoto hawa wanakuwa katika kipindi hisishi cha mota-neva. Kundi la pili (utoto wa kati) ni la watoto kuanzia miaka 2-6. Watoto katika kundi hili wanakuwa katika kipindi cha kabla ya utendaji. Kundi la tatu (utoto mpevu) ni la watoto wenye miaka 7-11. Kundi hili la watoto linakuwa katika kipindi cha utendaji-thabiti wa

mawazo. Kundi la nne (balehe) ni watoto wa miaka 13-16. Watoto katika kipindi hiki huanza kuingia katika hali ya utu uzima yaani kiakili, kimwili na kiumbo. Kwa hiyo, kwa mujibu wa mtaalamu huyu, mbali na mabadiliko ya ukuaji wa mwili, kuna mabadiliko ya uelewa na utambuzi wa mtoto kwa kila hatua. Ngugi na Wenzake (2019) wanafafanua kuwa kila kipindi ni muhimu kwa mtoto kwa sababu humsaidia kujifunza mambo muhimu hatua kwa hatua. Hoja yao inatokana na ukweli kuwa mtoto anapokua kuna mabadiliko mengi yanayotokea hasa katika fikra, lugha, hisia na maumbile. Kwa hiyo, mabadiliko haya hubadilisha tajriba na muono ulimwengu wa mtoto huyo.

Makala hii imebaini kuwa wahusika watoto katika filamu teule wanapitia changamoto za ukuaji hususani kwa kuruka hatua muhimu au kutojihusisha na tajriba muhimu za kundi la utoto walilomo. Hali hii inatokana na maelezo ya watoataarifa wanapoelezea jinsi walivyokuwa wanazingatia muda wao wa kufanya shughuli za filamu kando ya shughuli nyingine za kijamii kama kushiriki michezo na masomo. Maelezo yao yanadhihirisha kuwa watoto wanakosa tajriba za kundi-rika lao. Jambo hili huwafanya waanze kutengeneza uhusiano wa karibu na watu wanaowazunguka hususani walio katika tasinia yao bila kujali rika. Mtoataarifa ambaye ni MT 2 anasema:

Kwa ufupi kutengeneza filamu si suala dogo. Kuna masuala ya kukariri *script*, kufanya mazoezi na kuanza kurekodi ambapo hapo unakuta mnarudia zoezi mara kadhaa. Unaweza kuona jinsi ambavyo ni shughuli yenye kuhitaji muda mrefu. Kwa hiyo, mara nyingi shughuli za filamu tulikuwa tunazifanya wakati wa likizo au ikitokea dharura tulikuwa tunafanya muda wa jioni baada ya masomo. Hivyo, mara nyingi nilikuwa nawa*miss* marafiki zangu wa shuleni na mtaani. Ninachoweza kukumbuka ni kwamba baada ya kuanza kuigiza hata marafiki walinisahau kabisa. Baadae nilijikuta nawazoea wenzangu ninaofanya nao shughuli za kifilamu ambao hata hatulingani umri lakini ndo hivyo tunaanza kuitana *bro* basi maisha yanaenda. (Chanzo: mahojiano na mtoataarifa, 27/11/2023)

Dondoo hili linaonesha kuwa wahusika watoto hawana muda wa kushiriki shughuli zinazofanywa na kundi-rika kutokana na kubanwa kwa shughuli za filamu. Matokeo yake, watoto huambatana na watu wazima kwa sababu ndio wanaowazunguka. Kwa mujibu wa Nadharia ya ya Saiko- Changanuzi, hali wanazopitia watoto katika kipindi chao cha utoto zina athari kubwa katika maisha yao ya utu uzima. Hivyo, wahusika watoto katika filamu za Kiswahili ambao pia ni miongoni mwa watoataarifa katika utafiti huu wameanza kujihusisha na filamu katika umri wa kuanzia miaka 6 hadi miaka 13. Kwa mujibu wa mawazo ya wanasaikolojia, watoto katika kundi hili wanaanza kuonesha ukomavu wa fikra na kujinasibisha na mitazamo ya watu wengine ikiwa ni pamoja na kujaribu vitu vipya (Huck, 1979). Maelezo haya yanaonesha kuwa watoto ni rahisi kuiga mawazo ya watu wazima wanaoambatana nao. Hali hii inaweza kuendelea hadi kufikia katika kundi la miaka kuanzia 13 na kundelea. Hii ina maana ya kwamba japokuwa mtoto anakuwa mdogo kiumri, lakini tayari anakuwa ameshajiona mtu mzima kiasi cha kuweza kufanya maamuzi mwenyewe. Hivyo, anakuwa na mwanya wa kujaribu baadhi ya tabia hatarishi kama ngono na pombe ama kwa kujua au kwa kushawishiwa. Mtoataarifa ambaye ni MT 3 akizungumzia uzoefu wa maisha yake ya uigizaji katika filamu anasema:

Wakati naanza kuigiza nilibahatika kupendwa sana na watu. Katika shughuli za uigizaji nilijikuta nakuwa karibu na wenzangu waigizaji hivyo, badala ya kujifunza nikaanza kuharibikiwa. Katika kipindi changu cha utoto sikuwa naelewa lolote. Nilichokuwa najua ukiambiwa kuna hiki unafanya tu kwa sababu ya utoto. Ninaweza kusema watu wanaotakiwa kutulinda hawatulindi kwa hiyo tunajikuta tunajifunza mambo mabaya kuliko mema. Yapo mambo mengi mabaya yaliyonitokea kipindi cha nyuma baadae nilikuja kugundua *how young I was*. (Chanzo; Mahojiano na mtoataarifa, MM3, 5/ 3 /2024).

Dondoo hili linaonesha jinsi mhusika mtoto katika filamu alivyoshindwa kutambua mpaka baina yake na watu wazima aliokuwa akiambatana nao. Muambatano huo ulileta athari hasi katika maisha yake. Tafiti zinaonesha kuwa wasanii wengi ambao ni maarufu katika tasinia ya muziki au filamu mara nyingi wanakumbwa na tatizo la ulevi, kutumia madawa ya kulevya pamoja na starehe zisizo na ukomo. (Carlton-Ford, 2009). Kutokana na hili wahusika watoto wanajikuta wameingia kwenye mkumbo wa tatizo mojawapo. Hali hii huwafanya kuonekana hawako katika hali ya utoto wala utu uzima.

Utafiti wa Merlock, (1984) na Snell, (2016) ulibaini kuwa, changamoto za ukuaji wanazozipata wahusika watoto katika filamu zinatokana na umaarufu wanaoupata watoto hivyo, kuanza kujiamini na kujisahau. Tofauti ya utafiti huu na utafiti wa Merlock na Snell ni kuwa utafiti huu umebaini kuwa changamoto wanazozipata wahusika watoto zinatokana na maudhui wanayoyawasilisha ambayo yanakuwa juu ya urazini wao, uhusika wanaouvaa na mandhari wanazotumia kuigizia. Aidha, suala la kutumia muda mwingi pamoja na waigizaji wenzao ambao aghalabu ni watu wazima linawafanya wahusika watoto kukosa muda wa kukaa na kundi-rika lao na kubadilishana mawazo na tajriba za makundi-rika. Kwa hiyo, utafiti huu umebaini kuwa suala la wahusika watoto katika filamu haliepukiki kwa kuwa ni muhimu katika kujadili masula mazito yanayoikumba jamii lakini ni muhimu watoto walindwe kimwili, kiakili na kijamii. Jamii iwaone wahusika watoto kama watoto hata kama wanaonekana kuigiza au kuambatana na watu wazima. Aidha, kwa kuwa hivi karibuni watoto wengi na wazazi wao wamekuwa wakivutiwa na suala la watoto kuigiza, ni muhimu serikali iimarishe na kutekeleza sheria za haki za watoto

ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku watoto kuonekana katika kumbi za starehe na matamasha yanayofanyika usiku, na kuimarisha taasisi au kitengo rasimi cha kusimamia sanaa na makuzi ya watoto.

### 4.2.3 Mhusika Mtoto Kujengewa Mtazamo Hasi na Jamii

Mtazamo ni jinsi mtu anavyoona au kuelewa maisha ya kile ambacho ni kizuri au kisicho kizuri (Kisurulia na Kawira, 2018). Katika jamii, mitazamo hutofautiana kulingana na tabia ya mtu inayohusisha matendo. Utafiti huu umebaini kuwa urazinishaji wa wahusika watoto husababisha mtoto kujengewa mtazamo hasi katika jamii. Hali hii inatokea baada ya maudhui fulani (mara nyingi ambayo ni hasi) kuwasilishwa na mhusika mtoto, na hivyo, jamii kusahau kuwa ile ni sanaa na si uhalisia. Hoja hii ilielezwa na mtoataarifa ambaye ni MF 1anayeeleza:

Mhusika mtoto anaweza asiwe na tabia anayoiigiza lakini jamii ikamchukulia katika mtazamo huo wa kitabia kulingana na uigizaji wake. Kwa mfano, akiigiza kama adui, jamii itamchukulia hivyo hivyo (Chanzo: mahojiano na MF 1, 10/1/2024).

Maelezo hayo yanaonesha kuwa urazinishaji wa mhusika mtoto katika filamu huweza kumfanya kuwa na tabia ambazo huifanya jamii kuwa na mtazamo hasi dhidi yake. Mathalani, matendo ya kichawi aliyoyadhihirisha mhusika mtoto na lugha isiyokuwa ya kawaida kwa mtoto katika filamu ya *This Is It* vilimfanya aanze kutengwa na watoto wenzake shuleni na nyumbani. MT 2 anafafanua:

Kwanza, nilikuwa mdogo, baada ya ile filamu kutoka, nilishangaa kila nikienda shule wenzangu wanaanza kunitenga. Nikirudi nyumbani hali inakuwa vilevile. Nilipomuuliza mama alinijibu kuwa ni kwa sababu ya filamu. Nilijitahidi sana kuzoea hali hiyo. Hata hivyo, hali hiyo baadaye iliisha. (Chanzo: Mahojiano na MT 2, 25/1/2024).

Dondoo hili linaonesha kuwa miongoni mwa athari hasi za urazinishaji kwa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili ni kujengewa mtazamo hasi katika jamii. Kwa hiyo, kutokana na maudhui ya kichawi na ukorofi aliyoyawasilisha MMT 2 ambayo kimsingi yako katika uhasi katika filamu tajwa hapo juu, japokuwa lengo lake lilikuwa kuwafunza watoto, yaliifanya jamii kuanza kumchukulia katika mtazamo huohuo wa uhasi.

Suala la uwasilishaji wa maudhui ambayo yanaleta mtazamo hasi kwa jamii hubebwa na wanajamii kwa kushindwa kutofautisha maigizo na uhalisia. Kwa hiyo, ni muhimu kwa wanajamii kutofautisha suala la uigizaji na uhalisia ili kuwaondolea mtazamo hasi wahusika watoto wanaoibuka kila siku na wanaohitaji kukuza vipaji vyao.

### 4.2.4 Kuandikwa Vibaya na Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari ni asasi muhimu sana katika kukuza na kueneza lugha yoyote ile hasa katika enzi ya utandawazi (Kandagor, 2013). Pamoja na ukweli huo baadhi ya vyombo vya habari hususani mitandao ya kijamii imekuwa ikitumiwa vibaya na wanahabari (Mushumbwa, 2022). Utafiti huu umebaini kuwa miongoni mwa athari hasi ya urazinishaji wa wahusika watoto ni kuandikwa vibaya katika vyombo vya habari. Kwa mfano, mtoataarifa ambaye ni MT 1 anaweka bayana kuwa miongoni mwa mambo waliyokutana nayo wahusika watoto katika filamu ni kutengenezewa habari za uongo tangu wakiwa watoto huku zikiambatana na picha zao. Mtoataarifa huyo anasema:

Mara nyingine unaweza kukuta kuna habari inayoandikwa, ya uongo, na inawekwa picha yangu wakati huo sihusiki na chochote. Mfano, katika mitandao ya kijamii watu wanatutumia vibaya, hali inayozua taharuki katika jamii kwa manufaa yao binafsi na kunichafua mimi. (Chanzo: mahojiano na mtoa taarifa MT 1, 10/1/2024).

Data hii inaonesha kuwa wahusika watoto huchafuliwa na vyombo vya habari kutokana na umaarufu unaotokana na uhusika wanaokuwa nao katika filamu. Miongoni mwa vyombo vya habari vinavyotumiwa ni mitandao ya kijamii. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa urazinishaji unawapatia watoto umaarufu unaokuja na atahri hasi kama vile picha zao kutumiwa na waandishi wa habari kwa lengo la kujipatia wafuasi na kuendeleza maslahi yao binafsi. Aidha, maelezo haya ya mtoa taarifa yanaonesha kuwa umaarufu wa mhusika mtoto katika filamu hutumiwa na baadhi ya vyombo vya habari kuandika habari za uongo kuhusu mhusika mtoto lakini zikiwa na picha zao. Kitendo cha kuonekana picha ambayo ni ya msanii mtoto maarufu kuambatana na taarifa mbaya kunazua taharuki katika jamii.

## 4.3 MJADALA MFUPI NA MAPENDEKEZO

Urazinishaji wa wahusika watoto umeonekana kuwa na athari ambazo zinaanzia pindi wanapotambulishwa katika tasinia ya filamu hadi utu uzima wao. Athari hizo huweza kuwa hasi na kuwa chanya. Mojawapo ya athari chanya ni kupata uwezo na maarifa ya uigizaji katika umri mdogo. Maarifa hayo huwasaidia kujipatia umaarufu na kupata pesa. Tafiti zinaonesha kuwa mara nyingi waigizaji wanaopata umaarufu wakiwa watoto wanawahi kuingia katika hali ya utu uzima na kukosa muda wa kufurahia utoto wao. Jamii pia inawapokea kama watu wazima hali inayowafanya wapate matatizo ya kisaikolojia kama vile wasiwasi unayotokana na hali ya kutojua kundi-rika lao pamoja na kupata ugumu wa kutimiza majukumu yanayowakabili ikiwamo kulinda hadhi ya umaarufu.

Makala hii inasisitiza kuwa athari chanya na za muda mrefu kwa wahusika watoto zinategemea msaada mkubwa wazazi, walezi, jamii, ushauri wa afya ya akili

ambayo itawasaidia katika kukabiliana na maudhui wanayoyawasilisha, kuwarahisishia uelewa wa mpaka wa mabadiliko kati ya utoto na utu uzima pamoja na kukabiliana hali ya umaarufu wa mapema.

## 4.4 HITIMISHO

Makala hii imebaini kuwa urazinishaji wa wahusika watoto katika filamu za Kiswahili una athari hasi na chanya. Athari hizi zimebainika kutokana na mawazo ya Saiko- Changanuzi kuwa matukio mbalimbali yana athari kubwa katika mwenendo wa mtu. Pia, mazoea yanajenga tabia fulani ambayo inaacha athari kwa mhusika. Watoto wanaoigiza katika filamu wanapata athari kutokana na mazoea yanayojengwa na uhusika wanaopewa. Athari zilizobainika ni chanya na hasi. Kwa upande wa athari hasi makala hii inatoa wito kwa watunzi wa filamu hasa wanapoona ulazima wa kuwatumia wahusika watoto ni vyema kuwapatia maudhui yatakayoimarisha urazini wao kwa makuzi na maendeleo yao mazuri ya baadae.

## MAREJELEO


- Beebe, J. (2004). "*Understanding Consciousness Throgh the Theory of Psychological Types*" katika.
- Cambray, J na L, Carter (Wah). *Analytical Psychology Contemporary Perspectives in Jungian Analysis*. Kur. 83-115. London and New Work. Taylor and Francis Group. Inapatikana katika https://doi.org/10.4324/9780203492048, imesomwa tar. 2/12/2023.
- Ekiru, S. (2018). "Uadilishaji wa Mtoto katika Ujenzi wa Jamii yenye Adili: Tathimini ya Hadithi za Watoto". Katika Kandagor, M na M. Mukuthuria. (wah). *Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo Yake*. Kur. 26-41. Dar es Salaam. TATAKI.
- Freud, S. (1900). *Interpretation of Dreams*. Vienna. Macmillan.
- Gaydos, L. (2023). *When I grow up…* I don't want to be broke: The problems with child actor trust fund requirements. *Family Court Review*, *61*(4), 918-936 inayopatikana https://doi.org/10.1111/fcre.12745 imesomwa tar 12/4/2024.
- Hunt, P. (1999). *Understanding Children's Literature*. *Key Essays from the International Companion Encyclopedia of Children Literature*. New York: Routledge.
- Kandagor, M. (2013) "Juhudi za Vyombo vya habari katika kukuza na kueneza Kiswahili Nchini Kenya". *Kioo cha Lugha*. *Juz, 10*(1) 65-74.
- Kasiga, G. (2022). Athari za Unaigeria katika Video za Nyimbo za Mziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania: Uchunguzi wa Video Teule. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa ajili ya Kutimiza Baadhi ya Masharti ya Shahada ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Dodoma. (Haijachapishwa).
- Kisurulia, S., & Kawira, S. (2018). Wahusika, Uhusika na Mtazamo katika Riwaya. *Mulika*, *1*(1), 1-20. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mbarouk, J. S. (1981). Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Watoto. Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Zanzibar. (Haijachapishwa).
- Merlock, K. J. (1984). Images of Children in American Film: A Socio-Cultural Analysis. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kutimiza Baadhi ya Masharti ya Shahada ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Bowling Green State (Haijachapishwa)
- Mlaga, W. K. (2017). "*Fasihi ya Elektroniki, Matokeo ya Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia*". Makala Iliyowasilishwa Katika Kongamano la II ya CHALUFAKITA, SUMAIT- Zanzibar, Tar, 3-5.
- Mlama, P. (2003). "Hali ya Sanaa za Maonesho Tanzania" katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: *Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Mumbo, C. K. (2013). "Urazini wa Mwafrika: Tafakuri za Kidrama". Katika Kandagor. M na M. Mukuthuria (wah), *Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo Yake*. Kur, 42-53. Dar es Salaam. TATAKI.
- Mushumbwa, A. R. (2022). "Makosa ya Lugha katika Vyombo vya Habari Nchini Tanzania": Uchunguzi wa Televisheni. *Nuru ya Kiswahili. Juzuu*, *1*(2), 135-163. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ngugi, P. M. Y., Lyimo, B. E., & Bakize, H. L. (2019). *Fasihi ya Kiswahili ya Watoto: Maendeleo, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: TATAKI.
- Okereke, E. G. (1997). "Raising Womens' Consciouness TowardsTransformation in Nigeria": *The Role of Literature*. Cambrige University Press.
- Piaget, J. (1970) "*The Stages of the Intellectual Development of the Child*". katika P.H. Mussen, na wenzake (wah), Reading in Child Development and Personality, 2nd edition, New York: Happer and Row.
- Seng, K. B., Park J., Hwang J., Hee-Jeong, Y., Young –Sork, K., & Geon, P. (2013). "How Does the Movie Affect Child Actors (Actress) On Piaget's Cognative Development Theory?" In Korean Academy of Child and Adolescent Psychiatry. Kur. 65-70 https://doi.org/10.5765/jkacap.2013.24.2.65
- Shule, V. (2004). Effectiveness of Video Film in Reducing Young Men's Gender Violence and Other HIV Risk Behavior. Tasnifu Iliyowasilishwa kwa ajili ya Kuakamilisha Masharti ya Shahada ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Snell, H. (2016). "Uses and Abuses of the Child Figure in *Slumdog* Millionaire and Vikus Swarup's *Q & A*". Katika *Adaptation*, *9*(2), 234–248, Inapatikana

https://doi.org/10.1093/adaptation/apw027 Ilisomwa tar 12.7.2023.
- Sousa, A. (2010). "Freudian Theory and Consciousness: A Conceptual Analysis. Seminer on Mind, Brain and Conciousness". *National Library of Medicine*. Kur. 201-217. Inapatikana https://doi.org/10.4324/9780203492048, Imesomwa tar. 2/12/2023.
- Traverso, A. (2005). "Migrations of Cinema: Italian Neorealism and Brazilian Cinema". In K. Wilson (Ed.), *Radical Fantasy: Italian Neorealism's Afterlife in Global Cinema*. Kur. 165-186. Inapatikana katika http://hdl.handle.net/20.500.11937/7255. Imesomwa tar 23/2/2024.
- Wasylkiw, L., & Currie, M. (2012). The Animal House effect: How university-themed comedy films affect students' attitudes. *Social Psychology of Education*, *15*, 25-40. https://link.springer.com/article/10.1007/s11218-011-9167-x

**Cite This Article:** Tuzo Peter Bitesigirwe, Aldin K. Mutembei, Edith Lyimo (2024). Athari za Urazinishaji wa Wahusika Watoto katika Filamu za Kiswahili. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 7*(12), 404-413.